# UQAB

## Jarida la



*Toleo 20 - Dhul Hijjah 1439 H / Septemba 2018 Miladi*

**Mazingatio Muhimu Katika Ibada ya Hajj**

**Magharibi ni Adui wa Waislamu na Wanadamu**

**Vijana Jiungeni Kwenye Mabadiliko ya Kweli ya Kiislamu**

**Furaha na Mafanikio Halisi**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi - Halaqa 16**

**SWALI/JAWABU: Kongamano la Urusi na Amerika Jijini Helsinki**




## Risala Kutoka kwa Mwanachuoni Mkubwa Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah Katika Siku Kuu ya Idd ul-Adha Yenye Baraka ya Mwaka 1439 H Ikiafikiana na Mwaka 2018 M

# Risala Kutoka kwa Mwanachuoni Mkubwa Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah Katika Siku Kuu ya Idd ul-Adha Yenye Baraka ya Mwaka 1439 H Ikiafikiana na Mwaka 2018 M





**Allahu Akbar, Allahu Akbar, Allahu Akbar, La Ilaha Ila Allah, Allahu Akbar, Allahu Akbar, Wa lilah Alhamd**

Kwa Umma wa Kiislamu ambao Allah ameukirimu na kuusifu kama:

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ
**"Nyinyi ni Umma bora uliotolewa kwa watu munaamrishana mema na kukatazana maovu na munamuamini Mwenyezi Mungu"** [Al-i-'Imraan: 110].

Kwa wabebaji ulinganizi, Mashabaab na Mashabaat wa Hizb ut Tahrir, wabebaji ulinganizi wasafi na wachaMungu, ingawa hatumtakasi yeyote mbele ya Allah, wale wanaozungumza maneno ya kheri na kutenda vitendo vyema, na kisha kama natija yake Allah akawasifu wale wenye sifa hizi:

وَمَنْ أَحْسَنُ قَوْلًا مِمَّنْ دَعَا إِلَى اللَّهِ وَعَمِلَ صَالِحًا وَقَالَ إِنَّنِي مِنَ الْمُسْلِمِينَ
**"Na ni nani aliyembora katika maneno kuliko yule alinganiaye kwa Allah na kutenda mema na akasema: "Hakika mimi ni miongoni mwa Waislamu"** [Fussilat: 33].

Kwa wale watukufu wanaozuru ukurasa wa Facebook ambao huuzuru kwa ajili ya haki na ukweli, wakitafuta kheri inayobebwa nao, kwa hivyo Allah awalipe kheri…

Kwa wote hao,
**Assalamu Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh**

Nawapongeza katika siku kuu hii ya Idd ul-Adhaa na Allah awakubalie amali zao njema. Namuomba Allah Subhaanahu kuikubali Hajj ya wale wenye kuitekeleza na kuifanya kuwa Hajj yenye kukubaliwa, na juhudi yenye kupokewa vyema na dhambi zenye kusamehewa. Na pia namuomba Allah Subhaanahu kuwapa Tawfiq wale ambao hawakufanya Hajj mwaka huu ili wafanye mwakani pamoja na kheri juu ya kheri, na Allah Sunbhaanau ndio mlinzi wa walio wema.

**Kaka na dada zangu wapendwa:** Idd inakuja mwaka huu huku kukiwa hakuna Khilafah. Hivyo basi makafiri wakoloni na vibaraka wao wanatucheza karata dhidi yetu na kuchochea mauwaji na umwagikaji wa damu katika nchi zetu. Uhalifu wao wa kinyama umeenea kuanzia katika mabomu mpaka katika makombora yenye maangamivu hadi katika silaha za kemikali … yote haya kupitia mikononi mwao na wakati mwengine kupitia mikononi mwa vibaraka wao. Kila uangaliako utaona damu ya Waislamu ikimwagwa kwa dhulma kutokana na uvamizi … Upande wa Mashariki ni Burma, na mnajua nini kuhusu Burma, hali ya Waislamu huko ni ya kuumiza moyo, kutokana na uhalifu wa Mabudha na unyama wao ambao hata mazimwi wa mwituni hawawezi kuyafanya hayo … Na mnaona Kashmir na uhalifu wa India huko … Upande wa Kaskazini mnaona Chechnya na Caucasus na kisha Crimea ambayo inaangamizwa kupitia mikono ya Urusi, ambayo imeizamisha katika uhalifu na damu … mkitembea upande wa mashariki hadi Turkestan Mashariki, mtaiona China na aina zake tofauti tofauti za ukandamizaji … mkitembea kusini na kufika katika ufuo wa bahari yake, mtakipata kitovu cha ardhi za Kiislamu, Ardhi Tukufu, Palestina, Qibla cha kwanza kati ya Vibla viwili mtawaona Mayahudi wakiinyakua na kufanya uhalifu na mauwaji, na kusikia maumivu ya Msikiti huo ukilalama kutokana na donda kubwa linaloufanya kusikika kana kwamba unapumua pumzi zake za mwisho.

Kisha Ash-Sham na mnajua nini kuhusu Ash-Sham, damu ina mwagwa katika kila upande, mauwaji ya kinyama yameenea takribani katika kila barabara na mitaa kutokana na dhalimu wa Ash-Sham, na nyuma na mbele yake ikiwa ni Amerika na wafuasi na waungaji mkono kutoka Urusi hadi Iran na kisha wanamgambo … Wote hawa ndio wanaochochea moto, mauwaji na umwagaji damu kwa kila mbinu ovu za mauwaji … Na hapa mauwaji ya Idlib yanazidi kasi kupitia umiminaji mabomu kinyama katika pande zote, na halaiki ya madhalimu kudhamini hilo, kwa mchanganyiko wa khiyana inayoizunguka … Kisha Iraq, dada ya Ash-Sham katika majanga na maafa … Mkienda upande wa kusini hadi Yemen, ambayo mwanzoni ilikuwa na furaha, mtaiona imekuwa na huzuni kutokana na majanga ya mapigano yaliyoanzishwa na nchi za kikafiri za kikoloni, ziliyoifanya kama uwanja wa mashindano baina yao juu ya mafuvu na damu zetu … mukielekea upande wa machweo, mtaiona Libya na mapigano kati ya Waislamu wenyewe kwa wenyewe. Kisha mukielekea Afrika ya Kati, mtaona kuwa Waislamu wamepata mateso na uharibifu na kumwagwa damu zao isiyokuwa na hatia; kuvurugwa kwa matukufu huko hakuelezeki … Kisha jirani yake Sudan, eneo lake la kusini limetenganishwa na kaskazini, ikiiwacha kidonda chake kikivuja damu. Kisha Somalia inayolia kutokana na uchungu mwingi na mapigano makali kwa miaka.

Majanga yote haya yako katika ardhi za Waislamu, ambazo miaka ya nyuma zilikirimiwa kwa Uislamu, bendera ya Uislamu, Adhana ya Uislamu, na uadilifu wa Uislamu … Lakini baada ya kuvunjwa Khilafah na kuondoka kwa Imam, ngao (al-Junnah), hali ilibadilika, Umma ukateseka na wakoloni makafiri na vibaraka wao watawala madhalimu wakashuka na kushirikiana nao dhidi yake. Pasi na kutaja majanga ya Waislamu

***Endelea Uk..3***



Email: info@uqab.or.ke

katika nchi za makafiri, ni mengi mno, mataifa hayo yanataka kuwatoa Waislamu kutoka katika ngozi yao (kitambulisho), kwa hivyo wanalishambulia vazi la Wanawake wa Kiislamu, na wanataka kunyamazisha sauti yao ya Adhana, na wanaeneza chuki dhidi yao katika mujtamaa zao, asasi zao za kijamii na hata juu ya barabara zao … Ni janga tangu kukosekana Khilafah, moja baada jengine, majanga yaliyo kusanyika yanayo muacha aliye mgonjwa kuchanganyikiwa.

**Kaka na dada zangu wapendwa:** majanga haya lau yangelisibu taifa lolote lingeporomoka, au lingekata tamaa na maisha, lau kungali kuwepo na maisha yaliyosalia … Ama kwa Umma wa Kiislamu, uko na Kitabu cha Mola wake na Sunnah za Mtume wake na hata miujiza ya viumbe ya usiku na mchana, ambayo yanaufanya kuwa mkakamavu wakati wa matatizo na subra yake haidhoofiki kwa migogoro, lakini huongeza nguvu juu ya nguvu na huongeza subra juu ya kujizatiti kwake na kufanya kazi yake kwa imara na njia bora na kumtegemea Mola wake kwa ikhlasi:
* Kutoka katika Kitabu cha Mola wake: aya ziko wazi katika hili:

فَإِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا * إِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا

“Kwa hakika, pamoja na uzito ni wepesi* Hakika, pamoja na uzito ni wepesi” [Ash-Sharh: 5-6],

حَتَّى إِذَا اسْتَيْأَسَ الرُّسُلُ وَظَنُّوا أَنَّهُمْ قَدْ كُذِبُوا جَاءَهُمْ نَصْرُنَا فَنُجِّيَ مَنْ نَشَاءُ وَلَا يُرَدُّ بَأْسُنَا عَنِ الْقَوْمِ الْمُجْرِمِينَ

**“Mpaka walipokata tamaa Mitume na kudhani kuwa wamekadhibishwa iliwajia wao nusra yetu, na tukamuokoa kila tuliyemtaka. Na wala hakuna wa kuirudisha adhabu yetu kwa watu waovu”** [Yusuf: 110],

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُمْ مَثَلُ الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِكُمْ مَسَّتْهُمُ الْبَأْسَاءُ وَالضَّرَّاءُ وَزُلْزِلُوا حَتَّى يَقُولَ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ مَتَى نَصْرُ اللَّهِ أَلَا إِنَّ نَصْرَ اللَّهِ قَرِيبٌ

**“Je, mwadhani kuwa mutaingia Peponi kabla haujawafikeni mfano wa wale waliokuwa kabla yenu? Walipatikana na shida (ufukara) na madhara (mwili) na wakatingishwa mpaka Mtume na waumini pamoja naye wakasema, ‘ni lini nusra ya Allah?’ Pasi shaka, nusra ya Allah iko karibu.”** [Al-Baqara: 214]

* Katika Seerah ya Mtume wake: yale yaliyomtokea Mtume wa Allah (saw) wakati wa mwaka wa huzuni, pindi Khadija (ra), mama wa Waumini alipofariki, na kisha kifo cha Abu Talib, aliyemsaidia Mtume wa Allah (saw). Kisha majibu mabaya kutoka kwa watu wa Taif, yaliyomuacha Mtume wa Allah (saw) akivuja damu. Na kisha mgogoro huu kuongezeka na kuafikiana kumuua Mtume wa Allah (saw). Kisha wao (Maquraysh) kumwandama hadi kwenye pango la Thaur, alipokuwa amejificha pamoja na rafikiye Abu Bakr, Allah awe radhi naye. Wao (Maquraysh) walisimama mbele ya mlango wa pango huku masafa kati ya Mtume wa Allah na wao yakiwa ni shubiri moja au machache zaidi … hii ilikuwa katika mkesha wa kuamkia siku hiyo, na siku moja au mbili baadaye Mtume (saw) akasimamisha dola mjini Madina na kuunyanyua muundo wake kuujaza ulimwengu kwa nuru na kutangaza Haki …

* Ama miujiza ya viumbe ya usiku na mchana, kukolea kwa giza la usiku hufuatiwa na mwanga wa macheo ya kweli, na hiyo ni alama kwa watu wenye akili.

Hivyo basi, Umma wa Kiislamu haukati tamaa na rehema ya Allah, na hutambua kwamba baada ya uzito huja wepesi, baada ya shida huja suluhu, na mwanga wa asubuhi hufuatwa na giza la usiku … Kwa hivyo hautingishwi na mitetemeko, bali unafanya kazi na kufanya kazi kwa ikhlasi kwa ajili ya Allah na ni mkweli kwa Mtume wa Allah … Haudhuriwi na wale wanaopotoka kutokamana nao au kupotea; wengi wao hawakubali lolote isipokuwa Uislamu kama badali …

**Kaka na dada zangu wapendwa:** makafiri wale wameshusha pumzi za afueni baada ya Khilafah kuangushwa, kwa hivyo wanafanya uhalifu wao huku wakisalimika, hakuna anaye simama dhidi yao au kuwazuia kutokana na uhalifu wao au kuwarudisha kwao … Wanafahamu kuwa ngao ya Waislamu imeondolewa, na wanafanya kila juhudi yao kuzuia kurudi kwake. Hii ni kwa sababu wanajua kwamba mtengezaji wa ngao hii ni Khilafah, hapa ndipo pale hifadhi na heshima ya Waislamu ilipo. Hii ndio sababu wanawaandama wafanyikazi wanaofanya kazi ya kusimamisha tena Khilafah.

Hivyo basi, Hizb ut Tahrir imekuwa ndio shabaha ya mishale ya makafiri wakoloni na vibaraka wao watawala katika mataifa ya Waislamu. Hizb imetiwa katika misukosuko tofauti tofauti na mateso yaliyopelekea Shahada kama natija ya njama za makafiri na majasusi wa madhalimu na chuki za waovu. Hizb imepigwa marufuku na kuzuiwa katika ulimwengu wa Kiislamu hata katika zile nchi ambazo ziko wazi kwa vyama vyenye muundo tofauti tofauti mithili ya Indonesia; chama kimepigwa marufuku huko! Pamoja na zile biladi zilizofungua milango yake kwa vyama vya kila aina, hata vile vipotofu, mithili ya Tunisia, chama hiki kilipigwa marufuku! Ama kwa wanachama wa chama hiki, wafungwa wa madhalimu wanazungumzia mateso yao. Wanateswa katika magereza membamba, na katika magereza mapana wanadhalilishwa. Sasa ni kwa nini haya? Ni kwa sababu ya kuzungumza neno la Haki, ambalo chama inalitangaza, na huwachoma zaidi kushinda upanga, kwa sababu hawana hoja ya kusimama mbele ya neno la haki. Allah awaangamize, wamepotoka kiasi gani?

**Kaka na dada zangu wapendwa:** majanga haya yaliyousibu Umma huu na wafanyikazi wa Khilafah ni mabaya mno, na lau kama Allah hakuifanya Idd iwe chimbuko la furaha na njia ya raha na furaha nyoyoni mwa Waislamu, na mafungamano mazuri ya kizazi, na Umma kueneza salamu na heri njema ndani yake. Lau si kwa ahadi ya Allah (swt) kwamba izza na utukufu itarudi tena kwa Umma huu … Na lau kama si kwa bishara ya Mtume (saw) ya kurudi kwa Khilafah … Na lau kama si

***Endelea Uk..4***

kwa kuwepo kwa chama chenye ikhlasi kwa Allah (swt), chenye ukweli kwa Mtume wa Allah (saw), kinachofanya kazi mchana na usiku, kikilingania na kumuomba Allah kufungua kupitia mikononi mwao wawe ndio wenye kusimamisha Khilafah na kurudisha izza ya Uislamu na Waislamu … pasi na mambo haya manne; ingekuwa vigumu kutabasamu, kwa sababu kuna donda moyoni, na tezi kooni, kutokana na majanga mengi yanayo wazunguka Waislamu mbele na nyuma, kulia na kushoto; Khilafah imetoweka kwa muda wa takriban karne moja. Waislamu wametawanyika na kugawanyika wakitawaliwa na wajinga (Ruwaibidha). Bila ya kutaja uvamizi wa wakoloni makafiri na washirika wao ndani ya mataifa na watu wake, kana kwamba nchi za Waislamu ni uwanja wa mizozo ya kumwaga damu zetu na kuchafua matukufu yetu.

Lakini, kwa ubaya wa majanga haya, Hizb ut Tahrir imedhaminiwa nusra ya Allah na kutimizwa kwa ahadi Yake na bishara ya Mtume Wake (saw). Haikati tamaa na rehema za Allah maadamu inafanya kazi ya kheri kwa idhini ya Mola wake. Chama hiki kinatambua kwamba wakati wa Khilafah umeandikwa Kitabuni. Kila siku inapopita inaifanya hii siku kukaribia zaidi. Chama mithili ya hiki hakiruhusu ukataji tamaa moyoni mwake na azma yake haidhoofiki na kujikakamua kwake hakuvunjiki, kwa idhini ya Al-Aziz Al-Hakim, bali mazito hukiongezea nguvu yake, kwani mazito ni katika mitihani ya wanaume, na wanachama wa chama hiki ni wanaume wa kikweli wanaomuomba Allah (swt) kuwafanya miongoni mwa wale ambao Allah (swt) amewazungumzia:

رِجَالٌ لَا تُلْهِيهِمْ تِجَارَةٌ وَلَا بَيْعٌ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ وَإِقَامِ الصَّلَاةِ وَإِيتَاءِ الزَّكَاةِ يَخَافُونَ يَوْمًا تَتَقَلَّبُ فِيهِ الْقُلُوبُ وَالْأَبْصَارُ...

"[Ni] wanaume ambao haiwashughulishi biashara wala mauzo kutokana na kumkumbuka Allah na kusimamisha swala na kutoa zaka wanaiogopa siku ambayo nyoyo na macho yatageuka [kwa hofu]" [An-Noor: 37]

Wanabeba ulinganizi huu kwa imani yao pamoja na baraka kutoka kwa Allah, na kwamba ulinganizi huu utainuka mikononi mwao, InshaAllah, na hapo ndipo ahadi ya Allah (swt) na bishara ya Mtume Wake zitakapotimia katika vigawanyo vitatu kwa Tawfiq (mafanikio) na nusra ya Allah:

* Kwanza: kurudi kwa Khilafah kwa njia ya Utume baada ya utawala huu wa kutenzana nguvu: Imam Ahmad, na At-Taylasi katika Musnad yake kutoka kwa Hadith ya Hudhayfah, amesema: "Mtume wa Allah (saw) amesema: «... ثُمَّ تَكُونُ جَبْرِيَّةً، فَتَكُونُ مَا شَاءَ اللَّهُ أَنْ تَكُونَ، ثُمَّ يَرْفَعُهَا إِذَا شَاءَ أَنْ يَرْفَعَهَا، ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةٌ عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ» ... "Kisha utakuwepo utawala wa kutenzana nguvu, na utakuwepo apendavyo Allah uweko, kisha atauondoa anapopenda kuuondoa, kisha itakuwepo Khilafah kwa njia ya Utume"

* Pili: kupitia kuing'oa dola ya Kiyahudi kwa mizizi yake. Muslim anasimulia katika Saheeh yake katika riwaya ya Abu Hurayrah, Allah awe radhi naye: Mtume wa Allah (saw) amesema:

«...لَا تَقُومُ السَّاعَةُ حَتَّى يُقَاتِلَ الْمُسْلِمُونَ الْيَهُودَ، فَيَقْتُلُهُمُ الْمُسْلِمُونَ» "Kiyama hakitasimama mpaka Waislamu wapigane na Mayahudi, na Waislamu watawauwa…" Na katika riwaya nyengine, Yeye (saw) amesema: «تُقَاتِلُكُمْ يَهُودُ، فَتُسَلَّطُونَ عَلَيْهِمْ» "Mayahudi watapigana na nyinyi, na nyinyi mutawatawala."

* Tatu: Katika kufunguliwa Roma, kwa idhini ya Allah,

Ahmad amesimulia katika Musnad yake na Al-Hakim, na ilirekebishwa na kuidhinishwa na Az-Zahabi kutoka kwa Abi Qabeel, aliyesema: Tulikuwa na Abdullah bin Amr ibn al-Aas: Akasema: Tulipokuwa pambizoni mwa Mtume wa Allah (saw) tukiandika, Mtume wa Allah (saw) akaulizwa: "Ni upi kati ya miji miwili utafunguliwa mwanzo: Kostantiniya au Roma?" Mtume wa Allah (saw) akasema: «مَدِينَةُ هِرَقْلَ تُفْتَحُ أَوَّلًا، يَعْنِي قُسْطَنْطِينِيَّةَ» "Mji wa Hiraqla ndio utafunguliwa mwanzo, yaani Kostantiniya". Kostantiniya ishafunguliwa, na Roma itafunguliwa, InshaAllah.

**Kaka na dada zangu wapendwa:** kwa kutafakari hayo ya juu kwa akili timamu na ufahamu wenye hekima ni matarajio baada ya uchungu, na raha na bishara njema baada ya uhalisia wenye huzuni, na wepesi baada ya uzito, na furaha baada ya mateso ya muda mrefu, na kushuka kwa dua na rehema za Allah baada ya "Sisi ni wa Allah na Kwake Yeye tutaregea" … Kisha kheri na nusra … kheri na nusra … kisha kheri na nusra.

[وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ * بِنَصْرِ اللَّهِ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ]
"Na siku hiyo watafurahia waumini. Kwa nusra ya Allah, humnusuru amtakaye na Yeye ndiye Mwenye nguvu Mwenye rehma" [Ar-Rum: 4-5]

Kwa kutamatisha, namuomba Yeye Subhaanahu kwamba Idd hii yenye kheri na baraka irudi tena hali ya kuwa Umma wa Kiislamu uko chini ya kivuli cha bendera ya Uqab ya Khilafah Rashida, bendera ya Laa Ilaha Illallah Muhammadur Rasulullah

Na namuomba Allah (swt) kwamba wanachama wa Hizb ut Tahrir wawe msitari wa mbele wa Umma huu, wakisimama nao chini ya kivuli cha Khilafah Rashida … Ama kwa wanachama waliofariki kabla ya kurudi tena kwa Idd hii, namuomba Allah (swt) kuwaruzuku sehemu chini ya kivuli chake siku ambayo hakutakuwa na kivuli isipokuwa chake Yeye (swt). Allah ni Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.


Katika tamati yangu ya mwisho, nawatumia salamu zangu, nawaombea Dua ya kheri kwenu nyinyi.

Wasalamu Alaikum Wa Rahmatullahi Wa Barakaatuhu.

Ndugu Yenu,

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**
**Amiri wa Hizb ut Tahrir**

# Mazingatio Muhimu Katika Ibada ya Hajj



Hajj ni miongoni mwa hukumu za faradhi katika Uislamu. Nguzo hii miongoni mwa nguzo tano za Uislamu hutakikana kutekelezwa mara moja katika kipindi cha uhai wa Muislamu aliyee baleghe au kuvunja ungo na kumiliki uwezo wa kugharamia safari. Ibada hii ilicheleweshwa katika kufaradhishwa hadi mwaka wa 9 Hijria. Hekima inayotajwa ya kucheleweshwa kwake ni kwa kuwa Makkah ilikuwa chini ya utawala wa kishirikina wa Qureish waliokuwa wakitufu Al-Ka'ba uchi na kuabudu masanamu. Baada ya Waislamu kuikomboa wakiongozwa na Mtume (saw) mwaka wa 8 Hijria ikasafishwa kutokana na uchafu wa masanamu na kujumuishwa katika utawala wa Kiislamu (Darul-Islam) ambayo makao makuu yake ilikuwa ni Madinatul Munawwarah.

Watu wengi hasa vijana hughurika na uhai wakawa licha ya kuwa na uwezo wa kwenda Hajj wao hujijjengea dhana kwamba watahijii wakiwa wazee! Hufikiria kwamba ujana hupelekea mtu kuchuma madhambi mengi hivyo Hajj itakuwa haina maana katika ujana wake. Hii ni dhana potofu na hatari mno kwani Uislamu umetaka wafuasi wake wafanye haraka katika kutekeleza faradhi na amali njema kwa ujumla. Umri wa mwanadamu ni sekunde, dakika na masaa hivyo mja ataelekea kwa Mola wake ajali yake ikifika. Hakuna nafsi yoyote itakayocheleweshwa wala kutangulizwa ajali yake ikifika.

**عن ابن عباس رضي الله عنهما قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: تعجلوا الى الحج فَإِنَّ أحدكم لا يدري ما يعرض له**

Amepokea Imam Ahmad na Abu Daud kutoka kwa Ibn Abbas (ra) Alisema: Amesema Mtume Rehma na Amani za Mwenyezi Mungu zimshukie: 'Fanyeni haraka kuhiji kwani kihakika mmoja wenu hajui kile atakachokumbana na chenye kumzuia' (kutekeleza Hajj)

Ibada ya Hajj kama ilivyo ibada ya Saum bali na ibada nyengine za kiroho zimekutanishwa na suala la kumuogopa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu akasema kuhusu saum:

**..يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كتب عليكم الصيام كما كتب على الذين من قبلكم لعلكم تتقون**

**Enyi Mlioamini: Mumefaradhishiwa saum kama ilivyofaradhishwa kwa waliokuwa kabla yenu ili mupate kumcha Mwenyezi Mungu.** [Al-Baqarah: 183].

Akasema Mwenyezi Mungu kuhusu Hajj.

*Endelea Uk..6*

ذَٰلِكَ وَمَن يُعَظِّمْ شَعَائِرَ اللَّهِ فَإِنَّهَا مِن تَقْوَى الْقُلُوبِ

**Ndio hivyo! Na anayetukuza ibada za Mwenyezi Mungu, basi hayo ni katika unyenyekevu wa nyoyo.** [Al-Hajj: 32]

Hapa tunakuta kuwa asili ya Mwenyezi Mungu kutuamrisha sisi kumuabudu Yeye ni kuzatiti fungamano letu na Yeye na wala haina maana kwamba Yeye ni mhitaji wa ibada zetu kwani yeye amejitosheleza na wala haitajii chochote kuzidisha ufalme wake. Aidha inamaanisha kuwa tunatakikana kuhakikisha ibada hizi tunapozitekeleza zinatufikisha katika uchajiMungu wala sio kujifanyia tu…

Waislamu wanapohijii hutekeleza Hijja kwa udhati wake yaani kwa lengo la kupata thawabu tu wala sio kupata faida za kidunia. Kwa maelezo mengine ni kuwa Hajj shabaha yake ni kupata radhi za Allah pekee wala sio kupata manufaa ya kiulimwengu. Ndio,yawezekana Muislamu kupata ndani ya Hajj manufaa ya kidunia lakini hili sio kusudio la ibada ya Hajj bali ni ruhusa tumepewa na MwenyeziMungu ya kutafuta manufaa baada ya kutekeleza Hajj kwani kuna kukutana na watu mbalimbali. Anasema Mwenyezi Mungu:

لِّيَشْهَدُوا مَنَافِعَ لَهُمْ

**Ili washuhudie manufaa yao** [Al-Hajj: 28]

Ufahamu huu wa ufaradhi wa Hajj ni muhimu sana kwani sheria za Kiislamu hugawanyika katika mafungu mawili:- Sheria ambazo zilizo faradhishwa kwa lengo tu la kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu wala hakuna lengo lolote linalotakikana kupatikana hapa duniani. Hajj, Swala na Saum ni mifano ya ibada zilizo faradhishwa kwa Waislamu kwa dhati yake yaani kwa lengo tu la kupata thawabu pasina na kupata malengo ya kimada…

Kisha kuna sheria ambazo zilifaradhishwa sio kwa kujikurubisha tu kwa Mwenyezi Mungu bali kutekelezwa kwake kupelekee kupatikana malengo maalumu hapa duniani. Mfano kwa wakati huu ambao Waislamu wanaishi chini ya tawala za Kikafiri, Waislamu wanapobeba da'wah wasiibebe tu pasina kuwa na malengo ambayo sio kupata thawabu tu bali pia kuhakikisha Uislamu udhidhiri juu ya Dini zote nayo ni kwa kusimamisha Dola hapa duniani. Hivi ndivyo (saw) alivyobeba ulinganizi ambapo alikuwa na malengo ya kufanya Uislamu utawale. Na ndio (saw) alipoona mujtamaa wa Makkah umekataa Uislamu akaandaa mujtamaa wa Madinah ambao hatimaye ukakubali Uislamu na Mtume (saw) akasimamisha Dola yake huko. Hivyo hivyo sheria ya Jihadi, Waislamu hawapigani kwa lengo tu kupata shahada bali pia kuhami damu za Waislamu dhidi ya maadui wanapovamia ardhi yao na kuondosha vikwazo vinavyozuia kuenezwa Uislamu katika dunia ili walimwengu wote wapate kutekeleza maishani mwao uadilifu wa Uislamu. Kukata mwizi mkono ni sheria ambayo inafikisha katika lengo la kuhifadhi mali.…

Sio vyema kuzungumzia ibada tukufu pasina kugusia suala la umoja ambalo hudhihirika kila Mahujaji wanapokutana katika biladi tukufu Makkah hasa kisimamo cha Arafa. Kisimamo hiki hukumbusha umoja wa Umma kuwa ni Umma mmoja wa Kiislamu ambao Mwenyezi Mungu (swt) anawakumbusha waja wake:

(وَإِنَّ هَٰذِهِ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَأَنَا رَبُّكُمْ فَاتَّقُونِ)

**Na kwa yakini huu Umma wenu ni Umma mmoja, na Mimi ni Mola wenu Mlezi, basi niogopeni Mimi** [Al-Muminuun: 52]

Hukumbusha pia kauli yake (saw) katika kusifu mujtamaa wa Madina pale alifika ndani yake kwa kusema

"هذا كتاب من محمد النبي (رسول الله) بين المؤمنين والمسلمين من قريش وأهل يثرب ومن اتبعهم فلحق بهم وجاهد معهم...إنهم أمة واحدة من دون الناس"

Huu ni waraka wa Muhammad nabii na Mtume wa Mwenyezi Mungu baina ya Waumini na Waislamu wa Kiquraishi (Muhajiroon) na watu wa Yathrib (Ma-Answaar) na yoyote yule atakayejiambatanisha nao na akapigana Jihad pamoja nao : 'Hakika wao wote ni umma mmoja tofauti na watu wengine

Huu ni ukumbusho kwa mahujaji kuwa Umma huu umefungamanishwa imara na fungamano sahihi la kimfumo nalo ndio fungamano pekee linalodhaminia umoja wa Umma daima dawamu. Kwa namna basi mafungamano yote ya kirangi, kizalendo, kitaifa na kikabila yote ni mafungamano duni na Uislamu umekataza Waislamu kujifunga nayo. Fauka ya yote hayo ummoja huu ni lazima uwe chini ya kiongozi mmoja Khalifah ambaye ataulinda na kumpiga vita kila mwenye kutaka kuuvunja ummoja huu. Na kwa kuwa leo Umma hauna Khilafah basi Hajj yapaswa itiechachu kwa Waislamu jumla kufanya kazi ya kurudisha maisha ya Kiislamu kwa kuisimamisha Khilafah itakayoenzi umoja huu.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari Hizb ut Tahrir Kenya**

**Afisi kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 31/1439 | Ijumatatu, 02 Dhul Hijjah 1439 H | 13/08/2018 M

# Nyuma ya Shambulizi la Bomu la Nuklia Jijini Nagasaki Magharibi ni Adui wa Waislamu na Wanadamu

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Mnamo 9/8/2018, Japan iliadhimisha miaka 73 ya waathiriwa wa bomu la atomiki lililoangushwa na Amerika juu ya Nagasaki wakati wa siku za mwishoni mwa Vita vya Pili vya Dunia. Takriban watu 74,000 walifariki kutokana na athari ya bomu hilo, huku bomu lililolipiga jiji la Hiroshima mnamo 6/8/1945 likisababisha vifo vya watu 140,000 ambao walikadiriwa na Kanali wa Amerika Cunningham kuwa shabaha halali. Na hata kuwakadiria wakaazi wote wa Japan kama shabaha halali. Shambulizi hili la kinuklia ni kumbukumbu dhahiri ya kukosekana thamani ya kiakhlaqi, utu au ya kiroho katika sera za nchi za kikafiri za kikoloni. Itahitaji rekodi ndefu ndipo tuweze kuhesabu uhalifu uliojaa aibu uliotekelezwa na nchi za kimagharibi katika kampeni zao katili za kuukoloni ulimwengu katika karne zote zilizopita, pasi na kusaza sehemu yoyote ulimwenguni kutokana na uhalifu huu; tutataja baadhi ya uhalifu mkuu: vita vya kuangamiza wahindi wenyeji wa Amerika katika ulimwengu mpya (Kaskazini, Katikati na Amerika Kusini), au vita vya kufuja utajiri wa Afrika na kuwafanya watumwa watu wake, au vita maarufu vya opium ambavyo Uingereza (maarufu kwa msemo: “mzigo wa mzungu”) ilitaka kutajirisha hazina yake kwa gharama ya Wachina, moja kwa moja mpaka mabomu ya kinuklia ya Amerika yalioangushwa jijini Hiroshima na Nagasaki pasi na uhalali wa mkakati wowote wa kijeshi. Hii ni kupitia ushuhuda wa makamanda wakuu wa kijeshi nchini Amerika, akiwemo Jenerali Eisenhower kamanda wa majeshi ya Amerika barani Ulaya, na admirali William Halsey, waliosema, “bomu la kwanza la atomiki lilikuwa ni jaribio lisilokuwa na umuhimu… lilikuwa ni kosa… [wanasayansi] walikuwa na umbile hili na walitaka kulijaribu, kwa hivyo wakaliangusha!”

Bila shaka, rekodi ya uhalifu wa Wamagharibi haukukomea hapa; historia ya Vietnam, vijiji na viungani inatoa ushuhuda wa kiwango hiki cha uovu wa Amerika ambao licha ya kusimamisha ile inayodaiwa kuwa sanamu ya uhuru katika kisiwa cha Ellis jiijini New York, viongozi wake wa kisiasa na kijeshi hawakupumzika wakifurahia vinyago vyao, ikiwemo silaha zilizopigwa marufuku kimataifa, kuanzia napalm hadi vita vya kemikali vya Agent Orange, ambazo zimepigwa marufuku karatasini pekee. Kinyume na hayo vita vya kisasa (kuanzia Vita vya Kwanza hadi Vita vya Pili vya Dunia) vimeona yale ambayo kalamu haiwezi kuyasifia katika maangamivu, yakiwemo mauwaji ya wafungwa waliojeruhiwa mahospitalini. Zaidi ya hayo kuanzisha vita kamili visivyo tofautisha kati ya mtoto au mwanamke, mzee au mwanamke, maisha ya mwanadamu hayana thamani mbele ya mashetani watu hawa, uhalifu wote huu unatekelezwa chini ya jina gani? Ili kupata maslahi ya kikoloni kwa warasilimali wachache wanaodhibiti nchi hii na watu wake!!

Hivyo basi, ni ajabu unaposikia au kusoma taarifa ya mmoja au mwengine katika watoto wa Waislamu akitoa mwito kwa “jamii ya kimataifa” kutekeleza uamuzi fulani kupitia Baraza la Usalama au Umoja wa Mataifa, ambazo huungana tu kwa ajili ya uovu na uhalifu. Ya hivi karibuni ni matakwa ya wanaoitwa “wawakilishi” wa upinzani wa Syria kutoka katika taasisi za kimataifa, na Baraza la Usalama kutia “shinikizo” kwa muuwaji wa serikali ya Damascus kuwaachilia huru wafungwa! Je, ni wajinga juu ya ukweli kuwa “jamii ya kimataifa” ndio ya kwanza kujua ukweli wa uhalifu wa Bashar na kabla yake babake Hafez aliyefariki, pamoja na uhalifu wa Sisi, na mithili yao ya watawala wa Waislamu wahalifu wasioheshimu mkataba wowote au mafungamano na waumini? Ikiwa hawajui hilo ni janga, na ikiwa wanajua, hilo ni janga kubwa zaidi.

Wakati umewadia kwa Ummah kutambua uhalisia wa mzozo uliomo ndani yake, ambao unaulazimisha kumtambua rafiki kutoka kwa adui: wakoloni Wamagharibi, pamoja na washirika wa Kirusi, ndio adui, na zana za kutekeleza sera za kimagharibi kutoka kwa taasisi za kimataifa na ile inayoitwa “jamii ya kimataifa” na “mamlaka ya kimataifa” zote ni zana hatari ambazo hazina budi kupingwa. Ni lazima tufanye kazi kuregesha uamuzi wa Ummah mikononi mwake. Haipaswi kuziruhusu dola za kiimla kuchukua udhibiti wa kadhia zetu au kupigia debe masuluhisho yake yenye sumu. Hili ni kwa kadhia zetu zote kuanzia Palestina hadi Syria, Sudan, Kashmir na nyenginezo.

**Dkt. Osman Bakhach**
**Mkurugenzi wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Vijana Jiungeni Kwenye Mabadiliko ya Kweli ya Kiislamu

Tokea zamani nchi nyingi duniani zimekuwa zikiwawinda vijana kwa njia mbalimbali kama vile kuwatia tamaa na matarajio ya uongo pamoja na ahadi zenye matumaini wasiyotekelezewa daima.

Wakati tarehe 12 Agosti ya kila mwaka imechaguliwa kuwa Siku ya Vijana Kimataifa, hali ya vijana kiulimwengu ni mbaya, wengi wao wamekosa matumaini ya kuishi kamwe! Mfumo kandamizi wa kibepari unaowasimamia wanadamu kwa sasa umewatelekeza vijana kiasi cha kufikia wengine kuchukua maamuzi magumu kama kujiua, kutumia matumizi ya madawa ya kulevya nk.

Ujana ni hidaya na amana ajaaliwayo mwanadamu na Muumba wake. Ni katika wakati huu mwanadamu huwa na uwezo mkubwa wa nguvu za kiwiliwili na uwezo mkubwa wa kiakili na tafakuri. Ujana hufananishwa na jua la mchana ling'aapo, na uzee huchukuliwa kama jua lituapo ukihusishwa na udhaifu. Zaidi ya hayo, mambo mengi ya faida au hasara hufanyika wakati wa ujana, wanavyuoni wengi waliitafuta na kupata elimu yao katika umri wa ujana. Kwa mfano, Mwanachuoni, mwanasiasa na mujtahidi mkubwa wa zama hizi sheikh Taqiuddin An-Nabahan (Allah Amrehemu) alikuwa tayari ameshahifadhi quran yote akiwa tu kijana wa miaka 12. Nabii Ibrahim (as) akiwa ni kijana mdogo tu aliweza kujadiliana kwa hoja na Mfalme Nimrudh na kumshinda, Nabii Yusuf (as) aliteuliwa kuwa msimamizi wa mazao ya kilimo nchini Misri akiwa ni kijana mdogo.

Hata hivyo, mfumo wa kibepari umemtupa kijana licha ya kuwa ni rasilimali nyeti kwa ustawi wa mwanadamu. Takwimu za mwaka 2015 za Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na Masuala ya Ajira (ILO) asilimia 25 tu ya waajiriwa duniani ndio vijana. Hii inamaanisha wengi wa waajiriwa ni watu waliovuka umri wa ujana, ilhali zaidi ya asilimia 43 ya vijana duniani hawana ajira. Katika nchi zinazoendelea ambazo ni makoloni ya mataifa ya kibepari ya kimagharibi asilimia 31 ya vijana wake hawana elimu ya kujitosheleza kuweza kuajiriwa.

Wimbi kubwa la kudai mabadiliko haramu ya demokrasia yaliyoitwa mapinduzi ya kiraia yaliyoanzia Tunisia na kuenea Bara Arabu na Mashariki ya Kati liliungwa mkono moja kwa moja na vijana. Ni vijana tena wa Kiislamu ndio washiriki wakubwa katika mapinduzi hayo ambapo walionesha ujasiri, ushupavu, muhanga mkubwa na moyo wa kufa na kupona katika kuona kwamba mabadiliko ya kiutawala yanatokea. Hata hivyo, kwa bahati mbaya sana mioyo yao ya mihanga yao ilisukumwa na utumwa wa fikra za kimagharibi za kidemokrasia na wakapambana kufa kupona kutaka mabadiliko haramu na hatari ya kidemokrasia. Mabadiliko yanayomfanya Allah (swt) asiwe na nafasi katika maisha yao. Ama huku ni kutumika vibaya mno kwa nishati na mihanga ya vijana wa Kiislamu.

Ni muhimu ifahamike kuwa uwezo mkubwa wa kufikiri, upeo wa udadisi na tafakuri pana ikiambatana na usimamizi mzuri wa kufinyangwa Kiislamu vipawa vya vijana wetu itapelekea uwepesi kwa vijana kuuona ukweli, kuifahamu haki na hatimaye kushikamana nayo. Historia inatudhibitishia ukweli huo. Tukiangalia wafuasi takribani wote wa mwanzo wa Mtume (saw) walikuwa ni vijana, na ndipo Mtume (saw) aliposema "walikuwa vijana ndio walionipokea na kunikubali lakini wazee walinikataa". Kwa kawaida wazee wengi huwa ni wazito kufanya maamuzi magumu na waoga sana kukubali mabadiliko.

Tunashuhudia katika kisa cha watu wa pangoni (Aswhabu-ul Kahf), walikuwa ni vijana walioachana na dini na mila potofu za kishirikina na kuchukuwa mabadiliko sahihi kwa kumkubali na kumuamini Mwenyzi Mungu mmoja wa haki, Allah (swt). Qur'an inatukumbusha kwa kauli yake (swt) Anaposema:

إِنَّهُمْ فِتْيَةٌ آمَنُوا بِرَبِّهِمْ وَزِدْنَاهُمْ هُدًى

"**Hakika wao walikuwa ni vijana walio muamini Mola wao Mlezi. Na Sisi tukawazidishia uwongofu**". [Al-Kahf: 13]

Wakati sasa umewadia kwa vijana wa Kiislamu kuunganisha nguvu zetu pamoja kwa kubeba fikra zitakazoleta mabadiliko halisi ya Kiislamu. Fikra zitakazo tukomboa na utumwa wa fikra na mfumo batil wa kibinadamu wa Urasilimali wa Kisekula na kutupeleka kuwa watumwa na watumishi kamili wa Allah (swt) peke yake. Ili kuutawalisha mfumo wa Kiislamu kwa walimwengu wote. Mfumo wa haki anao uridhia Muumba wetu.

**Mohamed Abdulla Mohamed**
**Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano Hizb ut Tahrir Tanzania**

# Furaha na Mafanikio Halisi



Jumla ya wanadamu kila umuonaye anakwenda mbio huku na kule. Si tajiri wala masikini iwe ni mchana au usiku wote wanajituma kupita maelezo wakitafuta furaha na mafanikio. Ili tupate kuelewa mbio zao ni lazima tupate maana halisi ya furaha na mafanikio. Na ili tupate maana ya sawa ya maneno haya hatuna budi kurudia itikadi ambayo ndiyo msingi wa kupima usahihi na ubatili wa maana ya neno lolote lile. Kwa kuwa sasa tunatawaliwa na mfumo wa kirasilimali unaotokamana na itikadi ya Usekula (kutenganisha dini na maisha) iliyo mchanganya mwanadamu kwa kutomjibia kikweli maswali yake msingi nayo ni nini ulimwengu, binadamu na uhai? Badala yake ikamuachia kila mmoja kujijibia mwenyewe anavyotaka kwa kipimo cha manufaa/maslahi. Itikadi hii ikampa mwanadamu nguvu na mamlaka ambayo asili ni ya Allah (swt). Nguvu hizi ni pamoja na kutunga sheria kwa mujibu wa akili yake finyu ili kusimamia mambo ya wanadamu jumla. Itikadi hii haikutosheka na kumpa mwanadamu mamlaka bali ili mfafanulia kuwa lengo la kuishi hapa duniani ni kushibisha matamanio ya kiwiliwili chako kwa kiwango cha juu uwezavyo.
Na kwamba furaha inatokamana na uhuru mwanadamu aliokuwa nao katika kufanya atakavyo wakati wowote. Na kwamba aliye fanikiwa ni yule aliyefikia upeo wa juu katika kushibisha matamanio yake!

Kwa maana hiyo, utawakuta wanadamu waliobeba itikadi ya kisekula wakienda mbio zisizo na kikomo wakiamini kuwa kufanya hivyo kutawawezesha kumiliki mali nyingi zitakazo wawezesha kukimu matamanio ya viwiliwili vyao na hatimaye kuwa na furaha na mafaniko. Lakini hali ni kinyume kutokana na kuwa itikadi hiyo inakwenda kinyume na maumbile ya mwanadamu. Hali ni mbaya na yenye kutamausha kwani wafuasi wa itikadi hii wamekuwa duni kuliko hata wanyama. Kwani kumeshuhudiwa watu wanaomiliki chungu ya mali/pesa lakini bado wanataka kuwaibia walala hoi, kunao ambao wamekuwa na mali/pesa lakini bado wana wasiwasi kwamba zitawaondokea na hivyo kila kukicha wanalaghai kuhakikisha wanaziongeza mali/pesa zao na wengine kufikia viwango hata vya kuwafanya wazazi wao (mama zao) kama wake zao, wengine watoto wao kama waume au wake zao! Nao wanaume wakiolewa na wanaume wenzao na ilhali wanawake wakiolewa na wanawake wenzao! Kwa muonekano wa nje wafuasi wa usekula wanaonekana kama watu waliostawi na wanaostahili kuigwa lakini kwa sura ya ndani ni watu waliokata tamaa na maisha na waliojawa na msongo wa mawazo kupindukia kiasi kwamba wengine hufikia hata kujiua kwa mikono yao!

Kwa upande wa pili; tunayo Itikadi ya Uislamu (hapana Mola apasaye kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu na Muhammad ni Mtume wake). Itikadi hii Imemtatulia mwanadamu maswali msingi yanayohusiana na ulimwengu, mwanadamu na uhai pale ilipoeleza kwamba nyuma ya vitu hivi kuna Muumba naye ni Allah (swt). Na kwamba vyote

*Endelea Uk..10*

viko ndani ya nidhamu maalumu ambayo kila kimoja chake kamwe hakiwezi kujiondosha bali vyote vinamuhitajia Yeye Allah (swt). Na Mwenyezi Mungu kampa mwanadamu jukumu la kufanya ibada ndani ya umri wa maisha yake. Ibada kwa maana ya kujifunga na maamrisho na kujiepusha na makatazo ya Mwenyezi Mungu mahali popote wakati wowote. Na lengo la kuishi duniani ni kwa ajili ya Uislamu na kazi ya kila siku ni kuulingania Uislamu. Ama furaha ya mwanadamu inatokana na kujifunga na twaa ya Mola wake na wasiwasi (kutokuwa na furaha) wake unatokana na kwenda kinyume na maamrisho ya Mwenyezi Mungu. Na aliye fanikiwa ni yule aliyepata radhi za Mola wake na afe akiwa ni Muilsmu kivitendo na kauli huku akiwa na matarajio ya kuingizwa peponi adumu humo milele kwa Rehema za Mola wake Mlezi. Ama kipimo ni halali na haramu na kwamba natija ya kudumu katika kutenda halali kunapelekea mwanadamu kuwa na sifa ya uchajiMungu.

Kwa masikitiko makubwa, hivi sasa Waislamu licha ya kuwa na itikadi safi itokayo kwa Mola wao aliyewaridhia katika Uislamu wao. Bado wengi wao ni mateka wa itikadi hii mbovu ima kwa kujuwa au kutojuwa. Kwa sababu wamezaliwa, wamelelewa na wamekulia ndani ya dola hizi za kikoloni zinazoendeshwa na mfumo wa kirasilimali wa kisekula ambao umewafanya wao kuufahamu Uislamu kimakosa na hivyo kuzidi kutumbukia na kubakia katika kiza cha usekula ambacho daima kinawatawala hadi sasa. Wamefahamu ibada kama suala la mtu binafsi na lililofungwa msikitini au nyumbani kwa mtu binafsi. Hivyo basi Muislamu huyu anakuwa mkali kafiri akitaka kumswalisha lakini Muislamu huyu anapotoka nje ya msikiti anampa uongozi na kujisalimisha kwa kafiri yule yule aliyempinga msikitini asimswalishe! Hatima yake ni Waislamu kuwa na maisha ya mbio usiku na mchana na huwezi jua tofauti ya Muislamu na Kafiri kwani wote wanakwenda mbio kutafuta furaha na mafanikio kwa mujibu wa mtizamo wa itikadi ya Usekula.

La msingi na linalotakiwa kwa Muislamu hivi sasa ni kuliendea mbio usiku na mchana suala la namna gani atakavyoiregesha tena serikali ya Kiislamu ya Khilafah. Serikali ambayo iliangushwa 28 Rajab 1342H sawia na 3 Machi 1924 na maadui wa Uislamu kwa ushirikiano na wanafiki ndani ya serikali hiyo wakiongozwa na Mustafa Kamal. Kupitia kusimama serikali hii ndiyo Waislamu watafahamu maana halisi na kuipata ladha ya furaha na mafanikio kwa mtizamo safi wa Uislamu utakaokuwa unasimamiwa na kiongozi mchaMungu asiyejali mipaka ya kikoloni wala mafungamano ya kirasilimali ya kisekula. Waislamu watamiliki hadhi na cheo juu ya mgongo wa ardhi kinyume na hali ilivyo sasa ambapo licha ya kuwa na itikadi safi, wengi kiidadi na mali nyingi bado damu zao ni kama za kunguni zinamwagwa kiholela ulimwenguni kote kila sekunde. Chanzo kikubwa ni kukosekana kwa Serikali ya Kiislamu ya Khilafah itakayo washajiisha Waislamu kuwa wachaMungu kupitia sera ya elimu iliyo na lengo la kuwafinyanga Waislamu ili kuwa na Utambulisho wa Kiislamu.

Hadi pale ambapo Serikali ya Khilafah itakaposimama furaha na mafanikio itabakia kama kuutafuta unyoya wa mbu kwenye giza totoro. Isipokuwa wale ambao wamejifunga usiku na mchana katika Njia ya Mtume (saw) kuleta mageuzi juu ya mgongo huu wa ardhi wao pekee ndio wanaoifahamu furaha na mafanikio ya dunia hii kupitia kutumia mali/amana walizotunukiwa na Mwenyezi Mungu. Katika kufaulisha jambo hilo licha ya kuwa baadhi yao wamefungwa magerezani, wengine wakiwa katika hali ngumu zisizoelezeka na wengine wakipoteza maisha kamwe hawarudi nyuma katika ahadi walio muwekea Mwenyezi Mungu (swt) na Mtume wake (saw) bali daima wanasonga mbele wakiwa na yakini iko siku wataipata furaha ya kweli nayo ni kufa wakiwa ni Waislamu na ilhali wamedumu katika msimamo wao.

Namuomba Mwenyezi Mungu awazindue Waislamu wote ili wafahamu jukumu lililoko shingoni mwao kuhusiana na kazi ya kusimamisha Serikali ya Kiislamu ya Khilafah. Na hatimaye wajiunge na ndugu zao wanaharakati wa Hizb ut Tahrir katika kufanya kazi hii yenye malipo makubwa hapa duniani na akhera. Na ambao tayari wameshajiunga basi awadumishe katika khair hiyo hadi mwisho wa pumzi zao. Ama wasiokuwa Waislamu Mwenyezi Mungu awazindue wausome Uislamu kwa moyo mkunjufu na wauone kama ndio suluhisho badala ya mfumo wao wa kisekula wa kirasilimali. Allahuma Amiin!

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari Hizb ut Tahrir Kenya**



# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 16: Safari ya Mtume (saw) Kwenda Twaif Kutafuta Nusra Na Hifadhi Kutoka Kwa Thaqif

Katika Halaqa hii tutaangalia safari ya Mtume (saw) kuenda Taif akitafuta Nusra na hifadhi kutoka kwa Thaqif. Asema ibn Is'haq: Alipokufa Abu Talib, Maqureysh walimuudhi Mtume (saw) maudhi ambayo hakuyapata katika uhai wa Abu Talib.

Akatoka Mtume (saw) kwenda Taif kutafuta Nusra na hifadhi, na huku ana matumaini watamkubali na alichowajia nacho kutoka kwa Allah (swt), akawaendea akiwa peke yake, wakamjibu majibu mabaya kama utakavyoona mbeleni...!

Na hapa panahitajika ufahamu mzuri, na tuzingatie mazingatio ya hali ya juu, na tunafahamu kuwa nyuma tumeyagusia haya katika Halaqa ya utafutaji wa Nusra, na tunarudia kwa mara ya pili ili iwe msisitizo, nayo ni kuwa utafutaji wa Nusra unatakiwa uwe katika hali ya usiri mkubwa. Kwa sababu hiyo Mtume (saw) alikuwa anaenda peke yake ama na mmoja katika maswahaba zake ili watafute Nusra, ambayo inamaanisha usiri. Hii kazi haitakiwi mwengine ajue asokuwa katika viongozi...!

Na alipofika Mtume (saw) katika ardhi ya Taif akakusudia kipote miongoni mwa Thaqif ambao ndio mabwana wao na watukufu wao, nao ni ndugu watatu: Abdu Yalayl, na Mas'ud, na Habib, wakiwa na mwanamke mkureysh, akakaa nao na akawalingania kwa Allah (swt), akawaelezea aliyowajia nayo ya kumnusuru yeye na Uislamu, na kusimama pamoja naye kwa atakayemkhalifu katika jamaa zake.

Akasema mmoja wao: "Mimi nitaziiba nguo za Ka'bah iwapo Allah amekutumiliza na jambo lolote...!" Na akasema mwengine: "Kwani Allah ameshindwa kutuma mwengine asokuwa wewe...!?" Akasema wa tatu: "Wallahi sitozungumza na wewe baada ya kikao changu hiki kabisa; ikiwa wewe ni Mtume kama unavyosema, wewe unautukufu mkubwa na haki zaidi kuliko kusemeshwa na mimi! Na ikiwa unasema uongo dhidi ya Allah, basi wewe

Endelea Uk..12

ni muovu zaidi kuliko kusemeshwa na mimi! Na haitakiwi mimi nikuzungumzishe!" Akasimama Rasulullah (saw) ilhali amekata tamaa na kheri ya Thaqif, akawaambia: "**Ikiwa ndio hivyo mumeamua kufanya basi nifichieni!**"

Basi hawakulifanya hilo, bali waliwatuma wajinga wao na watumwa wao, wamtukane na kumpigia kelele mpaka wakamkusanyikia watu, wanamcheza shere Mtume (saw) wakamkalia safu mbili katika njia wakiwa wamebeba mawe, ikawa Mtume (saw) kila anapo nyanyua mguu wanampiga kwa mawe huku wanamcheza shere na kumdhalilisha...!

Alipowaondokea (saw), alikwenda katika ukuta wa shamba lao, akaja katika mti wa mzabibu akakaa chini yake ilihali ni mwenye taabu na maumivu, na miguu inachuruzika damu, kumbe katika shamba kuna Utbah na Shaibah watoto wa Rabia'h.

Alipowaona alichukia kuwaendea kwa kujua uadui wao kwa Allah (swt) na Mtume wake (saw), na watoto wa Rabia'h walikuwa wakimtizama, na wanaona wanachokifanya wajinga wa Taif. Alipotulia (saw), akaanza kumnog'oneza Mola wake na kuomba kwa Dua ambayo inazifungua nyoyo, na kurusha akili:

"**Ewe Mwenyezi Mungu! Nakushtakia Wewe udhaifu wangu, uchache wangu wa rasilimali na mahangaiko ninayopitia kutokana na watu. Ewe Mwenye Huruma katika walio na huruma. Ewe Bwana wa madhaifu na ambaye ni Bwana wangu. Umenielekeza kwa nani? Kwa mtu aliye mbali anayenipokea kwa uadui? Au kwa adui uliyempa mamlaka juu ya mambo yangu? Ikiwa hujanikasirikia basi mimi sijali. Ukarimu wako ni msaada mkubwa kwangu. Najilinda na mwangaza utokao Usoni Mwako ambao kiza chote huondoshwa na kila jambo katika hii dunia na ifuatayo huwekwa sawa, isije Hasira Yako au kutofurahishwa Kwako kukaniangukia mimi. Napenda furaha Yako na kutosheka kwako mpaka Uwe na furaha. Hakuna nguvu na uweza isipokuwa Kwako.**"

Mtume (saw) alifanya bidii kwa kila alichoweza, na kwa kila nguvu kutoka kwa Allah (swt), na Mtume (saw) hakubakia na chochote isipokuwa Nguvu za Allah (swt) ambazo hakuna nguvu inayoweza kulinganishwa nayo...!

ومن يتوكل على الله فهو حسبه

"**Na anayemtegemea Allah basi Yeye atamtosheleza**" [Talaq: 3]

Shayba na Utbah vijana wa Rabia'h walipoona yaliyompata Mtume (saw) waliguswa na huruma ya uzazi, wakamuita kijana mfanyikazi wao Mnaswara anaitwa: Addas, na wakamwambia: "Chukua hizi zabibu, weka kwa kibakuli, kisha umpelekee yule mtu, umwambie ale", Addas akafanya alivyoamrishwa. Akaenda na kuweka mbele ya Mtume (saw) kisha akamwambia: "Kula", Mtume (saw) alipoweka mkono wake alisema: Bismillah, kisha akala. Addas akamwangalia Mtume usoni kisha akasema: "Wallahi haya maneno hawayasemi kwa watu wa mji huu", Mtume (saw) akamwambia: "**Kwani wewe ni wa mji gani ewe Addas?**" Akasema: "Mie Mkiristo, na mimi ni mtu wa Ninawa", Akasema Mtume (saw): "**Ni katika mji wa mtu mwema Yunus bin Mattaa**" Addas akasema: "Umemjuaje Yunus bin Mattaa?" Akasema Rasulullah (saw): "**Huyu ni ndugu yangu alikuwa Mtume na mimi ni Mtume**". Addas akamwangukia Mtume (saw) huku anakibusu kichwa chake, mikono yake na miguu yake...!

Akasema mmoja katika watoto wa Rabia'h akimwambia mwenzake: "Ashamharibu kijana wako", aliporudi Addas walimwambia: "Ole wako ewe Addas! Una nini mbona wambusu huyu bwana kichwa chake, mikono yake na miguu yake...?!" Akasema, "Ewe bwanangu hakuna katika hii ardhi kitu bora kumliko huyu...! Amenipa khabari ya jambo hakuna alijuaye isipokuwa nabii…!" Wakamwambia, "Ole wako ewe Addas, asikuondoe katika dini yako, kwani dini yako ni bora kuliko yake…!"

# SWALI/JAWABU: Kongamano la Urusi na Amerika Jijini Helsinki

**Swali**

Maraisi wa Amerika na Urusi walifanya kongamano lao jijini Helsinki, mji mkuu wa Finland, mnamo Jumatatu 16/7/2018. Je hii ina maana kuwa taharuki kati ya nchi mbili hizi imekwisha? Je, kuna maana yoyote ya kufanywa kwa kongamano hili baada ya kongamano la nchi za NATO mnamo 12/7/2018 na taharuki iliyojitokeza kati ya Amerika na washirika wake wa Ulaya? Je, ina athari yoyote juu ya uhusiano wa Urusi na China? Je, kuna athari yoyote ya kongamano hili juu ya maamuzi nchini Syria?

**Jibu**

Katika kujibu maswali haya kuhusu kongamano la Amerika na Urusi jijini Helsinki, tunasema: kwamba baada ya takriban kipindi kirefu cha taharuki katika mahusiano kati ya Amerika na Urusi, iliyoanza mnamo 2014 wakati Urusi ilipoiunganisha Crimea nayo, na Amerika na Ulaya kujibu kwa kuiwekea Urusi vikwazo vya kiuchumi. Na taharuki kati ya nchi mbili hizi kuongezeka kwa kumalizika utawala wa Obama ambao uliituhumu Urusi kuingilia uchaguzi wa Amerika kwa manufaa ya mgombezi Trump, tangu wakati huo ilifutilia mbali kivitendo mikutano ya ngazi za juu kati ya pande mbili hizi … ingawa maraisi wawili hawa walikutana mara mbili kabla ya kongamano hili; walikutana pambizoni tu mwa kongamano la G20 mjini Hamburg, Ujerumani mnamo Julai 2017, na kukutana pambizoni mwa baraza la kikao cha ushirikiano wa kiuchumi (APEC) nchini Vietnam mnamo Novemba 2017.

Lakini, mikutano hiyo haikuinuka kufikia kiwango cha kongamano; ilikuwa ni mikutano mifupi na wala haikujadili kwa kina faili muhimu baina yao. Wakati wa kipindi cha mwaka mmoja na nusu cha utawala wa Trump, Urusi ilitafuta kwa ari kongamano baina ya maraisi hawa wawili, lakini Amerika ilikuwa ikiliakhirisha, na ilikuwa ikiuchukulia uakhirishaji huu kama mbinu ya kutilia shinikizo Urusi. Urusi imekuwa ikiusubiri mradi wa Trump ili kuimarisha mahusiano kati yao, lakini ilitambua ugumu wa kufanya hivyo kwa sababu ya wimbi kuu la upinzani katika upande wa Raisi Trump. Athari ya hili iliibuka wakati wa uchunguzi wa wazi dhidi ya Urusi na kujiuzulu kwa wanachama wa kundi la Trump juu ya madai kuwa na uhusiano na Urusi.

Hivyo basi, mkutano wa kiwango kikubwa katika ngazi ya kongamano umekuwa ndio ndoto kuu ya Urusi ambayo Urusi ilishindwa kuifikia. Iliwezekana tu baada ya Marekani kukubaliana nayo: "Msemaji wa Baraza la Usalama wa Kitaifa la Marekani Garrett Marquis alitangaza Alhamisi ya mwisho 21/6/2018 kuwa Mshauri wa Raisi wa Usalama wa Kitaifa, Bolton, atazuru Moscow mwishoni mwa mwezi huu na atajadili maandalizi ya kongamano kati ya Urusi na Marekani." Shirika la Kirusi la Sputnik 24/6/2018. Kwa hiyo, jambo muhimu zaidi kuzingatia katika kongamano hili, liliofanyika tarehe 16/7/2018 ni kwa nini Marekani iliamua (na sio Urusi) kuandaa kongamano kati ya marais hawa wawili, na nini inataka kupata kutokamana nalo? Ili kufafanua hili, tunasema:

1- Viashiria vyote vinaonesha kuendelea kwa shinikizo la Marekani juu ya Urusi. Siku mbili kabla ya kongamano hilo, Marekani iliwatuhumu maafisa wa kijasusi wa Urusi kwa kuhusika katika uharamia wa uchaguzi wa Marekani: "Idara ya Haki ya Marekani imewatuhumu maafisa 12 wa Kijasusi wa Urusi kwa udukuzi wa akaunti za maafisa wa chama cha Kidemokrasia wakati wa uchaguzi wa urais wa 2016, kwa mujibu wa Rod Rosenstein, naibu waziri wa haki, kwamba watuhumiwa walitumia jumbe za kupenyea zijulikanazo kama 'phishing' na barnamiji mbaya za komyuta ... Ikulu ya White House ilisema kuwa mkutano kati ya Trump na Putin Jumatatu utaendelea." Gazeti la Misri Al Ghad 14/7/2018. Mara baada ya Mkutano wa Trump na Putin kumalizika huko Helsinki, kituo cha runinga cha al-Jazeera kiliripoti mnamo tarehe 16/7/2018, tamko la Marekani la kukamatwa kwa mwanamke Mrusi huko Washington kwa mashtaka ya ujasusi kwa Urusi. Kwa vitendo hivi vilivyofanywa na mashirika ya serikali ya Marekani, kupunguza shinikizo kwa Urusi hakutarajiwi kuwa kama Urusi inavyotaka, licha ya kongamano hilo kati ya marais hawa wawili. Hii ina maana kwamba kuna sababu nyingine ambazo zimeisukuma Marekani kukubali ombi la zamani la Urusi la kutaka kongamano kati ya Maraisi Trump na Putin. Mambo haya yanadhihirishwa na dhurufu za kongamano hilo ...

2- Kongamano la Marekani na Urusi lilifanyika katika dhurufu ambayo Marekani imejiingiza vita vya kibiashara dhidi ya mahasimu wawili wakuu, Muungano wa Ulaya na China, na inaonekana kwamba Marekani iliamua kufanya kongamano hilo kwa kucheza kadi ya Urusi dhidi ya mahasimu hao wawili kwa pamoja!

Kuhusu Muungano wa Ulaya, Marekani ilichagua wakati wa kongamano hilo na Urusi punde tu baada ya kongamano la nchi za NATO, liliofanyika jijini Brussels huku kukiwa na sintofahamu kubwa kati ya Muungano wa Ulaya na Marekani. "Kongamano la NATO lilizinduliwa jijini Brussels leo huku kukiwa na matarajio kuwa litasheheni taharuki, hasa kati ya Washington na washirika wake wa Ulaya kwa msingi wa tofauti za kibiashara na matumizi katika ulinzi na makubaliano ya kinuklia ya Iran. Katibu Mkuu wa NATO Jens Stoltenberg

Endelea Uk..14

alikiri kuwepo kwa “sintofahamu na maoni tofauti miongoni mwa washirika’ (Russia Today, 11/7/2018), na Raisi wa Marekani Trump aliutaja Muungano wa Ulaya kama ‘mpinzani’ hadharani kwa mara ya kwanza katika historia ya mahusiano kati ya pande zote za Atlantiki. Kongamano na Urusi lilikuwa mojawapo ya ala muhimu zaidi ya shinikizo la Marekani dhidi ya Ulaya. Na hii ndio namna yake:

A- Raisi wa Marekani amewatishia Ulaya na rufaa ya Urusi kuhusu Ukraine, Raisi wa Baraza la Ulaya, Donald Tusk, alisema kuwa: “Raisi wa Marekani Donald Trump amemwambia kuwa madhumuni ya sera ya Urusi kwa Ukraine yalikuwa yanamvutia kwake, Trump alikiri kwamba shauku yake kwa Ukraine ni kidogo sana, Tusk aliongeza katika mahojiano yake na TVN24, kituo cha habari nchini Poland: “Katika mazungumzo kadhaa na mimi, Rais Trump hakuficha kwamba alihisi shauku kidogo kwa Ukraine na kuelewa zaidi ilichofanya Urusi nchini Ukraine,” (Russia Today, 15/7/2018) Hili ni jambo nyeti barani Ulaya. Ulaya imevitazama vitendo vya Ukraine kama vyenye kuingilia usalama wote wa Ulaya, hilo haliwezi kuvumiliwa, na taarifa ya Trump inachukuliwa na Muungano wa Ulaya kuwa ya hatari kwa Ulaya, inamaanisha kuwa Urusi yaweza kuharibu mpaka wa Ulaya na ramani kutoka upande wa mashariki!

B- Tishio la Raisi wa Marekani Trump kwa Ulaya la kuirudisha Urusi katika G7: “Rais wa Marekani Donald Trump siku ya Ijumaa, 8/6/2018, alitoa wito kwa wenzake wa G7 kuzingatia kurudi kwa Urusi katika kundi hilo. Trump alisema kabla ya kuelekea nchini Canada kushiriki katika kongamano la G7 huko La Malbaie katika jimbo la Quebec: “Waliitupa Urusi nje ... Wanapaswa kuiruhusu Urusi kurudi tena ndani, kwa sababu tunapaswa kuwa na Urusi katika meza ya majadiliano”. Urusi ilifukuzwa kutoka G8 baada ya kuiteka na kuiunganisha Crimea nayo na hivyo kundi hilo likajumuisha nchi saba tu.” (Chanzo: Al Arabiya.net, 8/6/2018).

C- Al-Jazeera iliripoti mnamo tarehe 15/7/2018, yaani baada ya kumalizika kwa kongamano la NATO (viongozi wa Ulaya wana wasiwasi juu ya maridhiano kati ya Urusi na Marekani). Kinachoashiria wasiwasi mkubwa wa Ulaya kuhusu maridhiano ya Marekani na Urusi ni kile alichosema Waziri wa Kigeni wa Ujerumani: “Heiko Maas, Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Ujerumani alimuonya Raisi wa Marekani Donald Trump juu ya mikataba yoyote ya upande mmoja kwa gharama ya washirika wake wa Ulaya wakati wa mkutano wake na Rais wa Urusi Vladimir Putin. Mass aliliambia gazeti la ‘Bild am Sonntag’: “Mikataba ya upande mmoja kwa gharama ya washirika itakuwa na madhara kwa Marekani, pia. Mtu anayewapiga washirika wake anajihatarisha hatimaye (Russia Today, 15/7/2018). Maridhiano kati ya Marekani na Urusi yanaweza kuharibu Muungano wa Ulaya, kama vikwazo vya Ulaya vilivyoekewa Urusi, ambavyo hufanywa upya kila baada ya miezi sita kwa sababu ya Crimea na Ukraine, vitadhaifishwa na hapo Urusi kutojali nchi za Ulaya basi.

D- Raisi wa Marekani Trump, ambaye amekosa hekima ya kisiasa, anaendelea kuushambulia Muungano wa Ulaya hadharani, hasa Ujerumani, juu ya kadhia ya ununuzi wa gesi ya Urusi, kama tulivyotaja katika jibu la swali la tarehe 17/07/2018 ... Wakati mwingine anautaja kama “hasimu” yaani “adui” na mara nyingine anachochea dhidi yake kama ilivyo katika ushauri wake kwa Waziri Mkuu wa Uingereza wakati wa mkutano wao wa jijini London: “Katika mahojiano na BBC, May alisema akijibu swali juu ya ushauri wa Trump alisema: “Aliniambia kuwa niushtaki Muungano wa Ulaya. Sio kuingia katika majadiliano” (BBC 15/7/2018).

Uingereza, licha ya kutangaza nia yake ya kujiondoa katika Muungano wa Ulaya, lakini ina maoni sawa na ya nchi za Ulaya juu ya Urusi, na hakuna uwezekano kwamba Uingereza kuichokoza Urusi ni kulivuruga kongamano kati ya Urusi na Amerika, “Tovuti ya Mil Radar, inayo shughulika na uchunguzi wa trafiki angani, iliripoti kuwa ndege ya upelelezi ya kikosi cha angani cha Uingereza ilifanya uchunguzi karibu na pwani ya Crimea ya Urusi.” (Russia Today, 15/7/2018).

Hivyo basi, kwa shinikizo la Marekani juu ya Ulaya na tishio lake la kuiregesha Urusi katika G7 na kudokeza kuitambua Crimea kama sehemu ya Urusi, na Marekani kutofautiana juu ya msaada wa Ukraine mbele ya shambulizi la wafuasi wa Urusi upande wa mashariki ( Donetsk na jimbo la Luhansk) na kuboresha uhusiano wa Marekani na Urusi kupitia kongamano hilo, ingawa si kwa njia ya moja kwa moja lakini ni tishio kubwa kwa Ulaya kwa haja ya kutimiza matakwa ya Marekani na kuongeza matumizi ya ulinzi katika NATO ... yaani, Marekani imezifinya nchi za Muungano wa Ulaya kupitia maridhiano yake na Urusi, na hii ni mojawapo ya malengo makuu ya Marekani ya kufanya kongamano kati ya Trump na Putin.

3- Kuhusu upande wa China, ni kama ifuatavyo:
A- Kongamano kati ya Marekani na Urusi pia lilifanyika nyuma ya vita vya kibiashara vinavyoongozwa na Marekani dhidi ya Beijing. Mara tu Marekani ilipokwisha tumia vya kutosha huduma za China kwa kupitia kulainisha msimamo wa Korea Kaskazini na kuiweka kwenye njia ya suluhisho ya amani na kuondoa tishio la vita kutoka katika bara la Korea. Hii iliwakilishwa na kongamano kati ya Marekani na Korea Kaskazini nchini Singapore tarehe 12/6/2018. Rais wa Marekani aliishukuru China kwa juhudi zake katika hilo. Mara tu baada ya matukio haya kufanyika, Marekani ilitekeleza sera zilizotangazwa na Trump dhidi ya China hata kabla ya kuwa raisi ... Marekani iliweka ushuru wa forodha kwa bidhaa za kutoka China wenye thamani ya dola bilioni 50 kwa mwaka, China ilijibu kwa kuweka ushuru wa forodha kwa thamani sawa kwa bidhaa kutoka Marekani. Marekani kisha ikatangaza mpango mpya wa kulazimisha ushuru wa forodha kwa bidhaa nyingine za

*Endelea Uk..15*

kutoka China wenye thamani ya dola bilioni 200, ambazo China haiwezi kwa njia hiyo hiyo, kwa sababu bidhaa zote jumla kutoka Amerika ni dola bilioni 130, huku bidhaa inazosafirisha kwenda Amerika ni dola bilioni 500, ambayo inasababisha China kufikiria njia nyingine za kukabiliana na vita vya kibiashara na Marekani.

B- Mojawapo ya njia hizi zilizochaguliwa na China ilikuwa ni maridhiano na Urusi. Shirika la Shanghai lilifanya mkutano wake wa mwisho nchini China mnamo 10/6/2018 kwa ushirikiano na mkutano wa nchi saba zilizoendelea-G7 (ambayo Urusi ilifukuzwa uanachama wake mwaka 2014) uliofanyika Canada mnamo 9/6/2018. Mikutano hii miwili imeonyesha mgawanyiko duniani. Magharibi inakutana nchini Canada na Mashariki inakutana nchini China, na hili halikupendelewa na Amerika baada ya kuanzisha utawala wake wa kiulimwengu baada ya kuanguka kwa Muungano wa Kisovieti mwaka wa 1991. Amerika iliona pasi na shaka kwamba nchi hizi mbili zilizochangamfu katika Shirika la Shanghai, China, ambayo Marekani imetangaza vita vya kibiashara dhidi yake, na Urusi, ambayo Marekani imeiwekea vikwazo vikali na vyenye kukua dhidi yake. Kwa upande mwingine, Amerika iliona kwamba Urusi na China zinaweza kutegemeana zaidi chini ya sera ya Marekani dhidi yao, kwa kuzichukulia kama mahasimu katika biashara na siasa za kimataifa, kwa mujibu wa sera hii ya Marekani kwa China na Urusi, Amerika imeona kwamba sera yake ina zisukuma nchi hizo mbili katika ushirikiano wa karibu, ikiwa upande wa kijeshi. Urusi na China zinahisi kuwa zinakabiliwa na adui mmoja, yaani Marekani, na kwamba ushirikiano wao unaimarisha nguvu zao. Ujumbe wa waziri wa ulinzi wa China uliweka wazi sana hisia hii. "Waziri wa Ulinzi wa Urusi Sergei Schweigo alimpokea mwenzake wa China, Wei Fenghe, ambaye aliwasili jijini Moscow kama kinara wa ujumbe wa kijeshi ili kushiriki katika kongamano la Usalama wa Kimataifa. Ujumbe wa China uliwasili ili kuwaonyesha Waamerika mafungamano thabiti kati ya majeshi ya China na Urusi, hasa katika hali iliyoko sasa." Waziri wa China alithibitisha: "Tulikusaidia. Upande wa China uko tayari kuonyesha, pamoja na upande wa Urusi, wasiwasi wetu na msimamo wetu wa pamoja juu ya masuala muhimu ya kimataifa.'' (Russia Today, 3/4/2018)

C- Hivyo basi Amerika iliona kuwa kufungua mlango kwa ajili ya maridhiano ya Urusi na Marekani kutapelekea kuwepo kwa utengano kati ya Urusi na China, na hatimaye kuvunja muungano wao tete kabla ya kumalizika kwa nguzo zake, hususan katika jeshi. Hii ni kwa sababu Amerika inatambua kile ilichonacho Urusi katika upande wa uwezo wa kijeshi, na kuziweka nguvu hizi au sehemu yake pamoja na China kutaipa nguvu na kuiruhusu kupinga sera ya Marekani, yaani, kutotimiza matakwa ya Washington. Washington ililiona hili kama jambo rahisi kulifanya.

Urusi inakwenda China kama mkakati mpya kwa sababu ya mahusiano yake duni na Magharibi. Ikiwa Marekani inaonyesha maridhiano yake na Urusi, shinikizo kwa Urusi itapunguwa na haitakwenda China.

Kwa sababu ya yote haya, Washington iliona kuwa ni sharti ifungue mlango wa matarajio kwa Urusi ili kuregesha mahusiano yake na Marekani katika msimamo uliokuwa mwanzoni kupitia kongamano hili baina ya maraisi wawili hawa, yaani, kuisitisha Urusi kwenda China. Ingawa ni mapema mno kuhukumu juu ya kupatikana kwa malengo haya ya Mrekani kutokana na kongamano hili pamoja na Urusi, na inategemea hatua za mbeleni za maridhiano kati ya Washington na Moscow, lakini Marekani yaweza kuuvunja kiurahisi "muungano" huo tete, mpaka kufikia sasa, kati ya Urusi na China. Marekani inachukua hatua kadhaa katika upande huu, baadhi ya wakati upande wa Urusi kama ilivyo katika kongamano hili, na baadhi ya wakati upande wa China. Kwani maslahi ya kibiashara ya China na Marekani yana kipaumbele kikubwa zaidi jijini Beijing kuliko uhusiano wowote ambao China iko nao na Urusi.

4- Kuongeza athari ya jumbe kali za Trump kwa Muungano wa Ulaya na China, Trump ililifanya kongamano hili kuwa mkutano wa wazi kulipeleka kila anapoona haja ya kulipeleka. Yaani ni mwanzo wa hatua zinazofuatia! Hivyo basi alisema baada ya mkutano wake wa faragha na Putin jijini Helsinki kuwa kongamano hili lilikuwa "mwanzo mpya" kwa mujibu wa kituo cha habari cha Urusi cha Russia Today mnamo 16/7/2018. Katika mkutano na waandishi wa habari uliopeperushwa moja kwa moja na Russia Today, alitangaza makubaliano kati ya nchi mbili hizo ili kuanza majadiliano juu ya kupanua makubaliano ya kusitisha silaha za kinuklia baina yao ya mnamo 2010, ambayo yatamalizika mnamo 2021, na Raisi wa Marekani Trump ametangaza kuwa mahusiano na Urusi yalikuwa katika hali mbaya baina yao masaa manne yaliyopita, lakini sasa hali imebadilika… Na haya yalikuwa mazungumzo jumla ambayo yanaafikiana barabara na yale yaliyotangazwa na John Bolton, Mshauri wa masuala ya Usalama wa Kitaifa wa ikulu ya White House aliyesema katika kipindi cha "This Week" katika kituo cha ABC network "Tumeomba, na Warusi wamekubali, kwamba kimsingi hayatakuwa na muundo. Sisi hatutafuti matunda thabiti," Balozi wa Marekani nchini Urusi, John Huntsman aliliambia shirika la habari la NBC: "Sio kongamano… ni mkutano… kwa hivyo hili ni jaribio la kuona kama twaweza kutatua na kuondoa baadhi ya visa, na kuweka wazi zaidi baadhi ya hatari, katika uhusiano huu kwa sasa. (Reuters, 16/7/2018)

5- Haya yanathibitisha kuwa Marekani bado haijapanga kuimarisha mahusiano yake na Urusi na ingali inafuatilia sera ya shinikizo juu yake. Lakini kwa sababu zihusianazo na hali ya kimataifa na vita vya kibiashara vya Marekani na Muungano wa Ulaya na China, ilitaka kuiogopesha Ulaya kwa maridhiano yake na Urusi.
Na iliamua kufungua nafasi ya matarajio kwa Urusi ya kukomesha kutengwa kwake kimataifa na ya kuimarisha

*Endelea Uk..16*

mahusiano yake na Marekani, yote ni kwa ajili ya kuiweka mbali na maridhiano na China kwa upande mmoja, na upande mwengine, Urusi huenda ikaitikia matakwa ya Marekani katika kadhia nyenginezo za kimataifa, kama ilivyo fanya katika kusaidia sera ya Marekani nchini Syria, kwa kuibakisha serikali kibaraka wa Marekani nchini Syria madarakani! Hivyo basi, kongamano hilo lilikuwa si la kutatua kadhia maalumu za kimataifa bali ni la kutuma ujumbe mkali ulioelekezewa China na Muungano wa Ulaya. Vyenginevyo, mazungumzo yalikuwa jumla na yalijadili kila kitu na sio vitu maalumu, kama ilivyothibitishwa na taarifa za pande zote mbili. "Trump alisema kuwa mazungumzo yake na Putin yatashughulikia "kila kitu, kuanzia biashara, masuala ya kijeshi, makombora, na "kumalizia" na China, tutazungumza kifupi kuhusu China na rafiki wetu wa pamoja, Raisi Xi" huku "Raisi wa Urusi Vladimir Putin akimwambia Raisi wa Marekani Donald Trump mwanzoni mwa kongamano lao jijini Helsinki kuwa wakati umewadia kuzungumza kuhusu mahusiano kati ya Moscow na Washington. Aliongeza kuwa pia wanapaswa kujadili kadhia nzito za kimataifa kati ya pande mbili hizo." (Reuters, 16/7/2018). Waziri wa Kigeni Sergei Lavrov alithibitisha kuwa kongamano hilo la Helsinki litazungumzia "kadhia zote nzito ambazo misimamo yetu inatofautiana ili tufanye kazi kuyaleta karibu maoni yetu kutatua matatizo haya," na akataraji kufikiwa makubaliano. (Tovuti ya Al Jazeera.net, 16/7/2018)

Ujumla huu unaonyesha nia ya kongamano hilo ya kutotatua kadhia za kimataifa, na hili liko dhahiri kutokana na matokeo ya kongamano hilo ambayo baadhi ya vyombo vya habari vimeripotia. Kwa mfano, pande mbili hizo zilikubaliana juu ya usalama wa umbile la Kiyahudi. Trump alisema "kutoa usalama kwa "Israel" ni jambo ambalo Putin na mimi tungependa kuliona sana." (Reuters, 16/7/2018) na kwamba pande mbili hizo zinataka Syria kurudi katika hali ya kijeshi iliyoafikiwa mnamo 1974 baada ya kumalizika kwa mapigano kusini mwa Syria … Yote haya si mageni, Marekani na Urusi zimekuwa zikiyasema hadharani kwa muda mrefu, hili si jambo ambalo viongozi wa Marekani na Urusi wanakutana kwa ajili yake. Hili ni sawia na kukomesha silaha za kinuklia baina ya nchi zao. "Raisi Donald Trump alisema kuwa tatizo la kukomesha silaha za kinuklia ni tatizo msingi ambalo halina budi kutatuliwa na Marekani na Urusi. Trump alisema katika mahojiano na shirika la habari la Fox News kuwa "asilimia 90 ya silaha za kinuklia ulimwenguni zinamilikiwa na Urusi na Marekani, akitaja kuwa mtangulizi wake, Raisi Barack Obama, alikadiria kuwa mvuke na viwango vya joto la kiulimwengu ndio tatizo muhimu mno, ambalo ni sharti liangaziwe." (Russian Today, 17/7/2018) … na kila mwenye maono anajua kuwa Marekani na Urusi hazikutani kukomesha silaha zao za kinuklia kwa khiari, lolote watakalosema, hivyo basi, mkutano wao si kwa lengo hili…

6- Ama kuhusu athari ya kongamano hilo juu ya uwanja wa Syria, inaweza kusemwa kuwa hakuna lolote jipya katika kongamano hili kuhusiana na sera za Marekani na Urusi nchini Syria. Nchi mbili hizi zinakubaliana kikamilifu juu ya kuyamaliza mapinduzi ya Syria, zote zinasubiri kupata hili pamoja na kukubaliana kikamilifu juu ya hilo, tangu baada ya mkutano kati ya Obama na Putin mnamo 29/9/2015, Urusi imetekeleza sera ya Marekani nchini Syria na kwa ushirikiano nayo, huku Urusi ikijihusisha na matendo ya moja kwa moja ya kijeshi kama umwagaji mabomu wa mji wa Daraa na viunga vyake, Marekani inaisaidia, kama ilivyo katika barua iliyotumwa kwa upinzani nchini Syria eneo la kusini, kuwa "Marekani haitawapa usaidizi wowote wakati wa shambulizi la Daraa." Hakuna jipya kuhusu juhudi za Urusi za kumaliza mapinduzi ya Syria kijeshi na urahisishaji wa Marekani kwa hilo.

Ama kuhusu suluhu ya kisiasa nchini Syria, Marekani inaiakhirisha mpaka serikali ya Damascus na Urusi zikamilishe mchakato wa kumaliza upinzani wa kijeshi. Hapo, ndipo Marekani itaongoza mchakato mpana wa kisiasa nchini Syria kwa mujibu wa maslahi yake, kwa dori ya Urusi au pasi kwa dori ya Urusi. Na mchakato huu wa kisiasa haukujadiliwa katika kongamano hilo ishara kuwa Marekani inauakhirisha au haitaki Urusi iwe na dori ndani yake, au yote mawili … Hakuna uwezekano kuwa Urusi inatambua kuwa malengo ya sera ya Marekani nchini Syria hayaruhusu Urusi kushiriki ndani yake, lakini Urusi inataraji kuwa Marekani haitaizuia nchini Ukraine, hususan Crimea… Trump aliifurahisha Urusi kwa matamshi yake kuhusu Crimea, kama ilivyo tajwa juu, alipotangaza katika kongamano la G7. Mwezi uliopita wa Juni vyombo vya habari vilitangaza kuwa Trump alitangaza wakati wa kongamano la G7 kuwa Crimea ni eneo la Urusi kila mmoja huko anazungumza Kirusi (Russia Today, 15/7/2018). Hii ni hatari mno kwa Ulaya, inayoamini kuwa Urusi inaharibu mipaka na ramani ya Ulaya kutokea upande wa Mashariki. Pengine Urusi itatumbukia ndani ya maangamivu yake kwa taarifa za Trump, na kwa hakika itatumbukia, na kufedheheka mbele ya Waislamu kutokana na uhalifu wake iliowafanyia dhidi yao kwa ajili ya maslahi ya Marekani! Na hili litabakia katika kumbukumbu ya Waislamu dhidi ya Marekani na Urusi na wapambe wao na wafuasi wao, kwa sababu zama zitabadilika, na uhalifu hautawaokoa wale walioutekeleza.

سَيُصِيبُ الَّذِينَ أَجْرَمُوا صَغَارٌ عِنْدَ اللَّهِ وَعَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا كَانُوا يَمْكُرُونَ

"**Utawafika wale waliohalifu udhalilifu mbele ya Allah na adhabu kali kutokana na vitimbi walivyokuwa wakivifanya**" [Al-An'am: 124]

**8 Dhul Qi'dah 1439 H**
**21/7/2018 M**